13

# TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA ZANZIBAR

# MWAKA, 2025

**27 JANUARI, 2026**

## TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA - ZANZIBAR KWA MWAKA, 2025

### UTANGULIZI

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu wa kuimarisha takwimu za jinsia nchini ikiwemo kukusanya na kuchambua takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu 21.

### LENGO


Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera nawatoa maamuzi.

### MATUKIO YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA YALIYORIPOTIWA POLISI MWAKA 2025

Jumla ya matukio 1,228 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwaka, 2025 ambapo waathirika walikuwa 1,230. Waathirika wengi walikuwa watoto (waathirika 1,050 sawa na asilimia 85.4), wakifuatiwa na wanawake 162 (asilimia 13.2) na wanaume 18 sawa na asilimia 1.5

Miongoni mwa waathirika watoto 1,050, wasichana walikuwa 942 (asilimia 89.7 na wavulana walikuwa 108 (asilimia 10.3).

**Kielelezo 1.1: Idadi ya Waathirika wa Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Mwaka 2025**



Idadi ya matukio ya kubaka yaliyoripotiwa yalikuwa 660, ambapo waathirika 600 walikuwa wasichana na 60 wanawake. Matukio ya Shambulio la aibu/kukashifu yalikuwa 166 ambapo waathirika 109 walikuwa ni wasichana, 50 walikuwa wanawake, watano (5) walikuwa ni wavulana na wawili (2) walikuwa ni wanaume. Matukio ya kutorosha yalikuwa 146 ambapo waathirika 140 walikuwa wasichana, watano (5) walikuwa wanawake na mwathirika mmoja (1) alikuwa mvulana. Matukio ya kulawiti/kunajisi yalikuwa 95 ambapo waathirika 91 walikuwa wavulana na wanne (4) walikuwa ni wanaume. Matukio ya kuingilia kinyume na maumbile yalikuwa 67 ambapo waathirika 60 walikuwa ni wasichana na saba (7) walikuwa wanawake.


**Jadweli 1.1 Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Aina ya Matukio Mwaka, 2025**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | Wanawake | Watoto | | Wanaume |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wasichana | Wavulana | |
| Kubaka | 660 | 60 | 600 | | |
| Kujaribu Kubaka | 5 | 3 | 2 | | |
| Kulawiti/Kunajisi | 95 | | | 91 | 4 |
| Kujaribu kulawiti/Kunajisi | 1 | | | 1 | 0 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 67 | 7 | 60 | | |
| Kutorosha | 146 | 5 | 140 | 1 | 0 |
| Lugha ya matusi | 47 | 20 | 18 | 8 | 2 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 166 | 50 | 109 | 5 | 2 |
| Kuingilia maharimu | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Uzinifu | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Usumbufu wa Kingono | 4 | 1 | 3 | 0 | 0 |
| Mauaji | 10 | 1 | 0 | 0 | 9 |
| Kutupa Watoto | 5 | 0 | 3 | 2 | 0 |
| Wizi wa Watoto | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 |
| Kutoa mimba | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 15 | 13 | 2 | 0 | 1 |
| **Jumla** | **1228** | **162** | **942** | **108** | **18** |

Wilaya Magharibi ‘A’ imeripotiwa matukio mengi, matukio 247 sawa na asilimia 20.1 ikifuatia Wilaya ya Magharibi ‘B’ ambayo imeripotiwa matukio 191 (asilimia 15.5).

Wilaya ya Kusini imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio, matukio 49 sawa na asilimia 4.0 ya matukio yote yaliyoripotiwa.

**Kielelezo 1.2: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Mwaka, 2025**



Idadi ya matukio ya udhalilishaji kwa mwaka yamepungua kwa asilimia 32.1 kufikia matukio 1,228 kwa mwaka 2025 kutoka matukio 1,809 yaliyoripotiwa Mwaka 2024. Matukio mengi yameripotiwa kupungua kwa mwaka 2025 isipokuwa matukio ya kutorosha ambapo pia baadhi ya matukio mapya yameweza kuripotiwa. Wilaya ya Magharibi ‘A’ ina idadi kubwa ya matukio kwa mwaka 2025 (matukio 247 ) ambapo wilaya ya Magharibi ‘B’ ilikuwa na idadi kubwa ya matukio mwaka 2024 (matukio 431).

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya na Aina ya udhalilishaji, Mwaka 2024 na Mwaka 2025**

| Wilaya | Idadi ya matukio | | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kujaribu kubaka | | Kulawiti/Kunajisi | | Kujaribu kulawiti/Kunajisi | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | |
| | Mwaka-2024 | Mwaka-2025 | Mwaka-2024 | Mwaka-2025 | Mwaka-2024 | Mwaka-2025 | Mwaka-2024 | Mwaka-2025 | Mwaka-2024 | Mwaka-2025 | Mwaka-2024 | Mwaka-2025 | Mwaka-2024 | Mwaka-2025 |
| Kaskazini 'A' | 59 | 72 | 37 | 45 | | 0 | 2 | 1 | | 1 | 2 | 0 | 8 | 14 |
| Kaskazini 'B' | 75 | 79 | 52 | 54 | | 1 | 13 | 6 | | 0 | 0 | 1 | 1 | 6 |
| Kati | 97 | 133 | 66 | 99 | | 0 | 12 | 7 | | 0 | 6 | 2 | 3 | 7 |
| Kusini | 46 | 49 | 21 | 33 | | 0 | 4 | 3 | | 0 | 5 | 0 | 4 | 6 |
| Mjini | 384 | 167 | 145 | 96 | | 0 | 32 | 21 | | 0 | 18 | 14 | 14 | 2 |
| Magharibi 'A' | 429 | 247 | 168 | 110 | | 2 | 35 | 13 | | 0 | 17 | 27 | 22 | 29 |
| Magharibi 'B' | 431 | 191 | 198 | 89 | | 0 | 37 | 20 | | 0 | 20 | 17 | 36 | 34 |
| Wete | 77 | 91 | 42 | 45 | | 1 | 8 | 6 | | 0 | 2 | 0 | 14 | 12 |
| Micheweni | 46 | 54 | 35 | 36 | | 0 | 6 | 4 | | 0 | 0 | 1 | 3 | 6 |
| Chake Chake | 113 | 93 | 49 | 28 | | 0 | 5 | 8 | | 0 | 1 | 0 | 25 | 27 |
| Mkoani | 52 | 52 | 21 | 25 | | 1 | 3 | 6 | | 0 | 0 | 5 | 9 | 3 |
| **Jumla** | **1,809** | **1228** | **833** | **660** | | **5** | **157** | **95** | | **1** | **71** | **67** | **139** | **146** |

**Inaendelea....Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya na Aina ya udhalilishaji, Mwaka 2024 na Mwaka, 2025**

| Wilaya | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Lugha ya matusi | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Kuingilia maharimu | | Mauaji | | Kutupa Watoto | | Wizi wa Watoto | | Kutoa mimba | | Kumpa na Kupokea ujauzito | | Uzinifu | | Usumbufu wa kingono | |
| | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 |
| Kaskazini 'A' | | 0 | 10 | 8 | 0 | | | 0 | | 0 | | 1 | | 2 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Kaskazini 'B' | | 0 | 9 | 10 | 0 | | | 0 | | 0 | | 1 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Kati | | 0 | 10 | 13 | 0 | | | 0 | | 3 | | 2 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Kusini | | 0 | 12 | 5 | 0 | | | 0 | | 1 | | 1 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Mjini | | 15 | 38 | 15 | 137 | | | 0 | | 0 | | 0 | | 1 | | 1 | | 2 | | 0 | | 0 |
| Magharibi 'A' | | 7 | 76 | 45 | 111 | | | 1 | | 2 | | 0 | | 0 | | 0 | | 9 | | 0 | | 2 |
| Magharibi 'B' | | 7 | 59 | 19 | 81 | | | 0 | | 2 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 1 | | 2 |
| Wete | | 14 | 11 | 9 | 0 | | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 4 | | 0 | | 0 |
| Micheweni | | 1 | 3 | 6 | 0 | | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Chake Chake | | 3 | 32 | 24 | 1 | | | 1 | | 2 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Mkoani | | 0 | 19 | 12 | 0 | | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Jumla | | **47** | **279** | **166** | **330** | | | **2** | | **10** | | **5** | | **3** | | **1** | | **15** | | **1** | | **4** |

***KUMBUKA: Matumio yenye rangi ya kijivu hayakuchambuliwa kwa mwaka 2024***

Miongoni mwa waathirika watoto 1,050 wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; Waliobakwa walikuwa wasichana 600, waliolawitiwa/kunajisi walikuwa wavulana 91, kuingilia kinyume na maumbile walikuwa wasichana 60, kutorosha walikuwa wasichana 140 na mvulana mmoja (1), shambulio la aibu/kukashifu wasichana 109 na wavulana watano (5).

**Jadweli 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto, Wilaya na Aina ya Matukio Mwaka, 2025**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kujaribu kubaka | Kulawiti/Kunajisi | Kujaribu kulawiti/Kunajisi | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | | Lugha ya matusi | |
| | | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 64 | 38 | 0 | 1 | 1 | 0 | 13 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 67 | 53 | 0 | 5 | 0 | 1 | 6 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 116 | 87 | 0 | 7 | 0 | 2 | 6 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 34 | 26 | 0 | 3 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 145 | 88 | 0 | 20 | 0 | 13 | 2 | 0 | 9 | 3 |
| Magharibi 'A' | 204 | 98 | 1 | 13 | 0 | 23 | 29 | 0 | 4 | 3 |
| Magharibi 'B' | 175 | 83 | 0 | 19 | 0 | 16 | 33 | 0 | 5 | 2 |
| Wete | 68 | 43 | 0 | 5 | 0 | 0 | 12 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 51 | 35 | 0 | 4 | 0 | 1 | 6 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 80 | 27 | 0 | 8 | 0 | 0 | 26 | 1 | 0 | 0 |
| Mkoani | 46 | 22 | 1 | 6 | 0 | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **1,050** | **600** | **2** | **91** | **1** | **60** | **140** | **1** | **18** | **8** |

Inaendele...... **Jadweli 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto, Wilaya na Aina ya Matukio Mwaka, 2025**

| Wilaya | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Kuingilia Maharimu | | Kutupa Watoto | | Wizi wa Watoto | | Kutoa Mimba | Kumpa na Kupokea Ujauzito | | Usumbufu wa Kingono | |
| | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 8 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 12 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 7 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 28 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 |
| Magharibi 'B' | 15 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Wete | 6 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 17 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **109** | **5** | **1** | **0** | **3** | **2** | **3** | **0** | **1** | **2** | **0** | **3** | **0** |

Miongoni mwa wanawake 162 ambao ni waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; waliobakwa walikuwa 60, , Shambulio la aibu/Kukashifu walikuwa 50, lugha ya matusi 20, kumpa na kupokea ujauzito 13, kuingilia kinyume na maumbile saba (7), kutorosha watano (5) na kujaribu kubaka watatu (3),pia kuingilia maharimu,mauwaji,uzinifu na usumbufu wa kingono yameripotiwa kuwa na waarika mmoja (1) kwwa kila tukio.

**Jadweli 1.4: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya Mwaka, 2025**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kujaribu kubaka | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Lugha ya matusi | Shambulio la aibu/Kukashifu | Kuingilia maharimu | Mauaji | Kumpa na Kupokea ujauzito | Uzinifu | Usumbufu wa kingono |
| Kaskazini 'A' | 9 | 7 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 9 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 14 | 12 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 15 | 7 | 0 | 0 | 2 | 0 | 5 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 21 | 8 | 0 | 1 | 0 | 3 | 7 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 41 | 12 | 1 | 4 | 0 | 0 | 15 | 1 | 0 | 8 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 13 | 6 | 0 | 1 | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Wete | 20 | 2 | 1 | 0 | 0 | 12 | 2 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 |
| Micheweni | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 11 | 1 | 0 | 0 | 0 | 3 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 6 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **162** | **60** | **3** | **7** | **5** | **20** | **50** | **1** | **1** | **13** | **1** | **1** |

Miongoni mwa waathirika wanaume 18 walioripotiwa mwaka 2025, mauaji walikuwa wanaume tisa (9), kulawiti walikuwa wanaume wanne (4), Lugha ya matusi wanaume wawili (2), Shambulio la aibu/kukashifu walikuwa wanaume wawili (2) na Kumpa na kupokea ujauzito alikuwa mwanamme mmoja (1).

**Jadweli 1.5: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanaume kwa Wilaya Mwaka 2025**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kulawiti | Lugha ya Matusi | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Kutelekeza Mtoto | Kuingilia Maharimu | Mauaji | Kutupa Watoto | Usafirishaji Haramu wa Binadamu | Kumpa na Kupokea Ujauzito | Udhalilishaji kwa njia ya Mtandao |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 3 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Magharibi 'B' | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 3 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **18** | **4** | **2** | **2** | **0** | **0** | **9** | **0** | **0** | **1** | **0** |

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 wameripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 618) sawa na asilimia 58.9 ya matukio yote ya watoto yaliyoripotiwa ikifuatiwa na umri wa miaka 11-14 (matukio 241) sawa na asilimia 22.9, umri wa miaka 6-10 (matukio 130) sawa na asilimia 12.4 na umri wa miaka 0-6 matukio 61 sawa na asilimia 5.8. Aidha matukio ya kubaka yanaonesha kuwa mengi zaidi katika umri wa miaka 15-17 (matukio 438) sawa na asilimia 73.0 kati ya matukio yote ya kubaka yalioripotiwa.

**Jadweli 1.6: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto na Umri Mwaka 2025**

| Umri | 0-5 | | 6-10 | | 11-14 | | 15-17 | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** |
| Kubaka | 11 | | 42 | | 109 | | 438 | | 600 | |
| Kujaribu Kubaka | 0 | | 0 | | 1 | | 1 | | 2 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 20 | | 33 | | 28 | | 10 | | 91 |
| Kujaribu Kulawiti/Kunajisi | | 0 | | 0 | | 0 | | 1 | | 1 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 4 | | 18 | | 20 | | 18 | | 60 | |
| Kutorosha | 0 | 0 | 1 | 0 | 30 | 1 | 109 | 0 | 140 | 1 |
| Lugha ya matusi | 0 | 0 | 0 | 1 | 7 | 4 | 11 | 3 | 18 | 8 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 15 | 3 | 33 | 2 | 40 | 0 | 21 | 0 | 109 | 5 |
| Kuingilia maharimu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| Usumbufu wa Kingono | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 3 | 0 |
| Kutupa Watoto | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 2 |
| Wizi wa Watoto | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 |
| Kutoa mimba | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 |
| **Jumla ya Waathirika** | **36** | **25** | **94** | **36** | **208** | **33** | **604** | **14** | **942** | **108** |

Idadi ya matukio ya watoto kwa mwaka yamepungua kwa asilimia 31.1 kufikia matukio 1,050 kwa mwaka 2025 ikilinganishwa na matukio 1,525 yaliyoripotiwa kwa mwaka 2024. Matukio mengi yameripotiwa kupungua kwa mwaka 2025 ikilinganishwa na mwaka 2024 isipokuwa matukio ya kutorosha.

**Jadweli 1.7: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri na Aina ya Matukio, Mwaka 2024 na Mwaka 2025**

| Miaka | Kubaka | | Kujaribu Kubaka | | Kulawiti/Kunajisi | | Kujaribu kunajisi/Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Lugha ya matusi | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Kuingilia maharimu | | Shambulio | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 |
| 0-5 | 29 | 11 | | 0 | 18 | 20 | | 0 | 7 | 4 | 2 | 0 | | 0 | 33 | 18 | | 0 | 0 | |
| 6-10 | 53 | 42 | | 0 | 63 | 33 | | 0 | 12 | 18 | 2 | 1 | | 1 | 87 | 35 | | 0 | 35 | |
| 11-14 | 169 | 109 | | 1 | 50 | 28 | | 0 | 20 | 20 | 25 | 31 | | 11 | 53 | 40 | | 0 | 72 | |
| 15-17 | 507 | 438 | | 1 | 22 | 10 | | 1 | 19 | 18 | 99 | 109 | | 14 | 51 | 21 | | 1 | 97 | |
| **Jumla** | **758** | **600** | | **2** | **153** | **91** | | **1** | **58** | **60** | **128** | **141** | | **26** | **224** | **114** | | **1** | **204** | |

***KUMBUKA: Matukio yenye rangi ya kijivu hayakuchambuliwa kwa mwaka 2024***


**Inaendelea.... Jadweli 1.7: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri na Aina ya Matukio, Mwaka 2024 na Mwaka, 2025**

| Miaka | Usumbufu wa Kingono | | Kutupa Watoto | | Wizi wa Watoto | | Kutoa mimba | | Kumpa na kupokea ujauzito | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 |
| 0-5 | | 0 | | 5 | | 3 | | 0 | | 0 | 89 | 61 |
| 6-10 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | 252 | 130 |
| 11-14 | | 1 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | 389 | 241 |
| 15-17 | | 2 | | 0 | | 0 | | 1 | | 2 | 795 | 618 |
| **Jumla** | | **3** | | **5** | | **3** | | **1** | | **2** | **1,525** | **1,050** |

***KUMBUKA: Matumio yenye rangi ya kijivu hayakuchambuliwa kwa mwaka 2024***


Matukio mengi (matukio 574) yametokea nyumbani kwa mtuhumiwa sawa na asilimia 46.7 ikifuatiwa na idadi ya matukio yaliyotokea majumba mabovu (matukio 164) sawa na asilimia 13.4 ikilinganishwa na maeneo mengine yaliyoripotiwa kwa mwaka 2025

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Sehemu Yaliyotokea, Mwaka 2025**




Muda uliyotokea matukio mengi zaidi ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia ni kuanzia saa 12:01 hadi 3:00 Usiku ambapo waliripotiwa waathirika 385 sawa na asilimia 31.3, ukifuatiwa na muda wa saa 9:01 hadi 12:00 Jioni waliripotiwa waathirika 307 sawa na asilimia 25.0 na muda wa 6:01 hadi 9:00 Jioni wameripotiwa waathirika 238 sawa na asilimia 19.3 ukilinganishwa na muda mwengine iliyoainishwa.

**Kielelezo 1.5: Idadi ya Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Muda Uliotokea, Mwaka 2025**





Matukio 540 kati ya matukio 1,228 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 44.0 ya matukio yote yaliyoripotiwa; aidha, matukio 396 yapo mahakamani (asilimia 32.2), matukio 95 yametiwa hatiani (asilimia 7.7),matukio 86 yamepewa hati ya mashtaka (asilimia 7.0), matukio 57 yamepelekwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (asilimia 4.6), matukio 35 yamefungwa na polisi (asilimia 2.9) na matukio 19 yameachiwa huru (asilimia 1.5).

**Jadweli 1.8: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Hatua Zilizochukuliwa Mwaka 2025**

| Aina ya Matukio | Idadi ya Matukio | Waathirika | | | | Hatua Zilizofikia | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Watoto | | Watu Wazima | | Zilizo Mahakamani | Zilizotiwa hatiani | Ziliachiwa huru | Zilizofungwa Polisi | Zilizopelekwa kwa Offisi ya M' mashtaka | Zilizo chini ya Upelelezi | Hati ya Mashtaka |
| | | Wasichana | Wavulana | Wanawake | Wanaume | | | | | | | |
| Kubaka | 660 | 600 | | 60 | | 211 | 66 | 15 | 25 | 40 | 241 | 62 |
| Kujaribu Kubaka | 5 | 2 | | 3 | | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 |
| Kulawiti/Kunajisi | 95 | | 91 | | 4 | 36 | 5 | 0 | 0 | 1 | 49 | 4 |
| Kujaribu kulawiti/Kunajisi | 1 | | 1 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 67 | 60 | | 7 | | 30 | 5 | 0 | 0 | 3 | 27 | 2 |
| Kutorosha | 146 | 140 | 1 | 5 | 0 | 51 | 12 | 1 | 8 | 5 | 62 | 7 |
| Lugha ya matusi | 47 | 18 | 8 | 20 | 2 | 15 | 4 | 0 | 0 | 0 | 28 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 166 | 109 | 5 | 50 | 2 | 43 | 3 | 3 | 1 | 8 | 97 | 11 |
| Kuingilia maharimu | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Uzinifu | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Usumbufu wa Kingono | 4 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 |
| Mauaji | 10 | 0 | 0 | 1 | 9 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 8 | 0 |
| Kutupa Watoto | 5 | 3 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 |
| Wizi wa Watoto | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Kutoa mimba | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 15 | 2 | 0 | 13 | 1 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 | 11 | 0 |
| **Jumla** | **1,228** | **942** | **108** | **162** | **18** | **396** | **95** | **19** | **35** | **57** | **540** | **86** |

Wafanyaji wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia walioripotiwa mwaka 2025 walikuwa 1,228 kati yao 491 walikuwa wapenzi sawa na asilimia 40.0, watu wasiojulikana walikuwa 320 sawa na asilimia 26.1, Jirani walikuwa 259 sawa na asilimia 21.1, watu wengine walikuwa 144 sawa na asilimia 11.7, Baba/Mama Mzazi/Kambo walikuwa 12 sawa na asilimia 0.9 na Mjomba/shangazi walikuwa wawili (2) sawa na asilimia 0.2.

**Kielelezo 1.5: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia Mwaka 2025**



## MAJALADA YA MAKOSA YA UDHALILISHAJI YALIYOPOKELEWA AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA ZANZIBAR MWAKA 2025

Jumla ya Majalada 599 yamepokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwaka 2025 ambayo yalihusisha makosa 648.Idadi kubwa ya makosa yaliyopokelewa yametokea Mkoa wa Mjini Magharibi (makosa 402) sawa na asilimia 62.0 ya makosa yote ikilinganishwa na mikoa mwengine.

**Jadweli 2.1: Idadi ya Majalada na Mkosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa Mwaka 2025**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Idadi ya Makosa |
|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 49 | 52 |
| Kusini Unguja | 77 | 78 |
| Mjini Magharibi | 363 | 402 |
| Kaskazini Pemba | 55 | 58 |
| Kusini Pemba | 53 | 56 |
| Makao Makuu | 2 | 2 |
| **Jumla** | **599** | **648** |

Kati ya Majalada 599 ya Udhalilishaji yaliyoripotiwa mwaka 2025, majalada 295 yameruhusiwa kwenda mahakamani sawa na asilimi 49.2, majalada 166 yamerudishwa Polisi kwa Upelelezi zaidi sawa na asilimia 27.7, majalada 127 yamependekezwa kufungwa sawa na asilimia 21.2 na majalada 11 hayajatolewa uamuzi sawa na asilimia 1.8.

**Jadweli 2.2 Majalada ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa na Hatua, Mwaka 2025**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Yalioruhusiwa kwenda Mahakamani | Yaliopendekezwa kufungwa | Yaliorudi Polisi kwa Upelelezi | Hayajatolewa Uamuzi |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 49 | 35 | 5 | 5 | 4 |
| Kusini Unguja | 77 | 48 | 15 | 13 | 1 |
| Mjini Magharibi | 363 | 154 | 89 | 114 | 6 |
| Kaskazini Pemba | 55 | 28 | 11 | 16 | 0 |
| Kusini Pemba | 53 | 29 | 7 | 17 | 0 |
| Mkao Makuu | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| **Jumla** | **599** | **295** | **127** | **166** | **11** |

Miongoni mwa makosa 648 ya udhalilishaji yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, makosa mengi zaidi yaliyojitokeza yanahusiana na kubaka (makosa 378) sawa na asilimia 58.3 ya makosa yote yaliyopokelewa.


**Jadweli 2.3: Idadi ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa, Mwaka 2025**

| Aina ya Makosa | Kaskazini Unguja | Kusini Unguja | Mjini Magharibi | Kaskazini Pemba | Kusini Pemba | Makao Makuu | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kubaka | 33 | 60 | 232 | 32 | 20 | 1 | 378 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 0 | 1 | 58 | 1 | 2 | 0 | 62 |
| Kulawiti/ Kunajisi | 1 | 6 | 31 | 5 | 6 | 0 | 49 |
| Ukatili kwa Mtoto | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 3 |
| Kutorosha | 8 | 2 | 21 | 7 | 8 | 0 | 46 |
| Kubaka kwa Nguvu | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Shambulio la Aibu/ Kukashifu | 5 | 8 | 51 | 11 | 15 | 1 | 91 |
| Kumuingilia Maharimu | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 2 |
| Kumuingilia Mnyama | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kujaribu Kubaka | 2 | 0 | 1 | 1 | 2 | 0 | 6 |
| Kuruhusu Kuingilia Kinyume na Maumbile | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kubaka kwa Kundi | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 3 |
| Unyonyaji wa Kingono | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Usambufu wa Kingono | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kujaribu Kulawiti | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Uzinifu | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Udhalilishaji mkubwa wa kingono | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| **Jumla ya Makosa** | **52** | **78** | **402** | **58** | **56** | **2** | **648** |

## MASHAURI NA MAKOSA YA UDHALILISHAJI YALIYOFUNGULIWA KATIKA MAHKAMA ZA UDHALILISHAJI ZANZIBAR KWA MWAKA 2025

Jumla ya mashauri 241 yanahusisha makosa 305 yamefunguliwa katika mahakama za udhalilishaji kwa mwaka 2025. Mkoa wa Mjini Magharibi umeripotiwa kuwa na mashauri mengi yaliyofunguliwa ambayo ni mashauri 131 (makosa 174) sawa na asilimia 54.4 ya mashauri yote ikilinganishwa na mikoa mengine.

**Kielelezo 3.1: Mashauri ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyofunguliwa kwa Mkoa Mwaka, 2025**



Kati ya mashauri 241 yalifunguliwa mahkama za udhalilishaji, Mashauri 159 bado yanaendelea sawa na asilimia 66.0, mashauri 29 yametiwa hatiani sawa na asilimia 12.0 na mashauri 53 hayana hatia sawa na asilimia 22.0.

**Jadweli 3.1: Idadi ya Mashauri ya Ukatili na Udhalilishaji Zilizofunguliwa katika Mahkama na hatua zilizochukuliwa Mwaka 2025**

| Aina ya Makosa ya Majalada | Zilizopokelewa | Zinazoendelea | Zilizotiwa hatiani | | | | | Zisizo na hatia | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kifungo | Faini | Fidia | Kifungo na fidia | Faini na fidia | Zilizoachiwa huru | Zilizondoshwa/Zilozfutwa |
| kubaka | 104 | 54 | 5 | 2 | 0 | 3 | 8 | 10 | 22 |
| Kubaka kwa kundi | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| kubaka na kutorosha | 14 | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 3 |
| kubaka na kumuingilia kinyume na maumbile | 30 | 26 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 |
| kubaka na kumuingilia kinyume na maumbile na kutorosha | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| kubaka na shambulio la aibu | 3 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Jaribio la kubaka | 3 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 21 | 21 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kuingilia kinyume na maumbile na shambulio la aibu | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kulawiti | 9 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 |
| kujaribu kulawiti | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| kulawiti na kutorosha | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| kulawiti na shambulio la aibu | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| kutorosha | 14 | 7 | 0 | 1 | 0 | 0 | 2 | 3 | 1 |
| Kutorosha na shambulio la aibu | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu | 28 | 22 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 4 |
| Kukashifu | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Shambulio la matusi | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ukatili kwa mtoto, | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kuingilia maharimu | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| kubaka mgonjwa wa akili | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Utelekezaji wa watoto | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **241** | **159** | **6** | **6** | **0** | **4** | **13** | **22** | **31** |

Jumla ya makosa 305 yaliyopokelewa katika Mahkama za udhalilishaji wa kijinsia , makosa mengi zaidi yaliyojitokeza yanahusiana na kubaka (makosa 154) sawa na asilimia 50.5 ya makosa yote yaliyopokelewa.

**Jadweli 3.2: Idadi ya Makosa ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia yaliyopokelewa Kimkoa Mwaka, 2025**


| Mkoa | Kaskazini Unguja | Kusini Unguja | Mjini Magharibi | Kaskazini Pemba | Kusini Pemba | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| kubaka | 20 | 34 | 80 | 13 | 7 | 154 |
| Kubaka kwa kundi | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Jaribio la kubaka | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 3 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 1 | 8 | 50 | 2 | 0 | 61 |
| Kulawiti | 2 | 2 | 7 | 0 | 1 | 12 |
| kujaribu kulawiti | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| kutorosha | 4 | 4 | 10 | 11 | 4 | 33 |
| Shambulio la aibu | 1 | 3 | 24 | 2 | 5 | 35 |
| Kukashifu | 2 | 0 | 3 | 0 | 0 | 5 |
| Kuingilia maharimu | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| **Jumla** | **32** | **51** | **174** | **30** | **18** | **305** |

## WANAFUNZI NA MAHABUSU WA MAKOSA YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA WA CHUO CHA MAFUNZO MWAKA 2025

Jumla ya Wanafunzi wa makosa ya udhalilishaji waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa Januari -Disemba, 2025 walikuwa 81 na Mahabusu walikuwa 202.


Wilaya ya Mjini imeripotiwa kupokea wanafunzi wengi (wanafunzi 19) ukilinganisha na wilaya nyengine, vilevile, mahabusu wengi wamepokelewa kutokea Wilaya ya Mjini (mahabusu 54).

**Kielelezo 4.1: Idadi ya Wanafunzi na Mahabusu Waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa Wilaya, Januari - Disemba, 2025**




Umri wa miaka 25-35 umeripotiwa kuwa na wanafunzi na mahabusu wengi zaidi ikilinganishwa na makundi ya miaka mengine (mahabusu 95 na kwa upande wa wanafunzi walikuwa 33).

**Kielelezo 4.2: Idadi ya Wanafunzi na Mahabusu Waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa Umri, Januari – Disemba 2025**



Wanafunzi wengi wamehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 11 nakuendelea (wanafunzi 30) sawa na asilimia 37.0 ikilinganishwa na vifungo vyengine.

**Jadweli 4.1: Idadi ya Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo kwa Muda wa Vifungo na Aina ya Makosa, Januari- Disemba, 2025**

| Muda wa Vifungo | Aina ya Makosa | | | | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | Kuingilia kinyume na maumbile | Kulawiti | Kujaribu kulawiti | kutorosha | Shambulio la aibu | Kukashifu | Shambulio | Kuingilia maharimu | |
| Chini ya miezi 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Miezi 4-11 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 6 | 0 | **9** |
| Mwaka 1-2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 11 | 0 | **12** |
| Miaka 3-5 | 0 | 1 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 15 | 1 | **20** |
| Miaka 6-10 | 3 | 2 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 2 | 0 | **10** |
| Miaka 11+ | 19 | 5 | 4 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | **30** |
| **Jumla** | **22** | **8** | **4** | **0** | **7** | **4** | **1** | **34** | **1** | **81** |

## HITIMISHO

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia, muda wa matukio yalipotokea na wafanyaji wa matukio. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu 21. Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

Jumla ya matukio 1,228 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwaka, 2025 ambapo waathirika walikuwa 1,230. Waathirika wengi walikuwa watoto (waathirika 1,050 sawa na asilimia 85.4), wakifuatiwa na wanawake 162 (asilimia 13.2) na wanaume 18 sawa na asilimia 1.5

Idadi ya matukio ya udhalilishaji kwa mwaka yamepungua kwa asilimia 32.1 kufikia matukio 1,228 kwa mwaka 2025 kutoka matukio 1,809 yaliyoripotiwa Mwaka 2024. Matukio mengi yameripotiwa kupungua kwa mwaka 2025 isipokuwa matukio ya Kutorosha.

Matukio 540 kati ya matukio 1,228 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 44.0 ya matukio yote yaliyoripotiwa; aidha, matukio 396 yapo mahakamani (asilimia 32.2), matukio 95 yametiwa hatiani (asilimia 7.7),matukio 86 yamepewa hati ya mashtaka (asilimia 7.0), matukio 57 yamepelekwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (asilimia 4.6), matukio 35 yamefungwa na polisi (asilimia 2.9) na matukio 19 yameachiwa huru (asilimia 1.5).

## Kiambatanisho

**Jadweli 1.0: Idadi ya Waathirika ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika na Aina ya Matukio Mwaka, 2025**

| Sehemu Zilotokezea | Nyumbani kwa Muathirika | | Nyumbani kwa Mtuhumiwa | | Nyumba za wageni/rafiki | | Sehemu za kazi | | Skuli | | Madrasa | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **W'ke/Ws** | **W'me/Wv** | **W'ke/Ws** | **W'me/Wv** | **W'ke/Ws** | **W'me/Wv** | **W'ke/Ws** | **W'me/Wv** | **W'ke/Ws** | **W'me/Wv** | **W'ke/Ws** | **W'me/Wv** |
| Kubaka | 22 | | 329 | | 41 | | 1 | | 0 | | 0 | |
| Kujaribu kubaka | 1 | | 2 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 6 | | 34 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Kujaribu kulawiti/Kunajisi | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 2 | | 42 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | |
| Kutorosha | 18 | 0 | 79 | 1 | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Lugha ya matusi | 17 | 2 | 13 | 5 | 0 | 0 | 4 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 29 | 0 | 45 | 3 | 4 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kuingilia maharimu | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Uzinifu | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Usumbufu wa Kingono | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mauaji | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kutupa Watoto | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wizi wa Watoto | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kutoa mimba | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 0 | 1 | 13 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **93** | **11** | **531** | **43** | **54** | **1** | **7** | **3** | **0** | **0** | **2** | **0** |

**Inaendelea….Jadweli 1.0: Idadi ya Waathirika ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika na Aina ya Matukio Mwaka, 2025**

| Sehemu Zilotokezea | Majumba mabovu | | Vichakani | | Vyombo vya usafiri(Gari) | | Fukwe za bahari | | Sehemu nyengine | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **W'ke/Ws** | **W'me/Wv** | **W'ke/Ws** | **W'me/Wv** | **W'ke/Ws** | **W'me/Wv** | **W'ke/Ws** | **W'me/Wv** | **W'ke/Ws** | **W'me/Wv** | **W'ke/Ws** | **W'me/Wv** |
| Kubaka | 99 | | 108 | | 1 | | 1 | | 58 | | 660 | |
| Kujaribu kubaka | 2 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 5 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 27 | | 13 | | 0 | | 0 | | 15 | | 95 |
| Kujaribu kulawiti/Kunajisi | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 1 | | 1 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 14 | | 2 | | 0 | | 0 | | 7 | | 67 | |
| Kutorosha | 9 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 24 | 0 | 145 | 1 |
| Lugha ya matusi | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 2 | 1 | 38 | 10 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 13 | 0 | 18 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 47 | 2 | 159 | 7 |
| Kuingilia maharimu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Uzinifu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Usumbufu wa Kingono | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 |
| Mauaji | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 1 | 9 |
| Kutupa Watoto | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 3 | 2 |
| Wizi wa Watoto | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 |
| Kutoa mimba | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 15 | 1 |
| **Jumla** | **137** | **27** | **136** | **16** | **2** | **1** | **3** | **0** | **139** | **24** | **1,104** | **126** |

**Jadweli 2.0: Idadi ya Waathirika ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Mwaka 2025**

| Wilaya | Kubaka | Kujaribu kubaka | Kulawiti /Kunajisi | Kujaribu kulawiti/ Kunajisi | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | | Lugha ya matusi | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Kuingilia maharimu | | Kutupa Watoto | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'ke/Ws | W'ke/Ws | W'me/Wv | W'me/Wv | W'ke/Ws | W'ke/ Ws | W'me/ Wv | W'ke /Ws | W'me/ Wv | W'ke/ Ws | W'me/ Wv | W'ke/ Ws | W'me/ Wv | W'ke/ Ws | W'me/ Wv |
| Kaskazini 'A' | 45 | 0 | 1 | 1 | 0 | 14 | 0 | 0 | 0 | 9 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 54 | 1 | 6 | 0 | 1 | 6 | 0 | 0 | 0 | 8 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kati | 99 | 0 | 7 | 0 | 2 | 7 | 0 | 0 | 0 | 13 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Kusini | 33 | 0 | 3 | 0 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Mjini | 96 | 0 | 21 | 0 | 14 | 2 | 0 | 12 | 3 | 14 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 110 | 2 | 13 | 0 | 27 | 29 | 0 | 4 | 3 | 43 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 89 | 0 | 20 | 0 | 17 | 34 | 0 | 5 | 2 | 18 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 45 | 1 | 6 | 0 | 0 | 12 | 0 | 12 | 2 | 8 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 36 | 0 | 4 | 0 | 1 | 6 | 0 | 2 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 28 | 0 | 8 | 0 | 0 | 26 | 1 | 3 | 0 | 24 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 25 | 1 | 6 | 0 | 5 | 3 | 0 | 0 | 0 | 12 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **660** | **5** | **95** | **1** | **67** | **145** | **1** | **38** | **10** | **159** | **7** | **2** | **0** | **3** | **2** |

**Inaendelea....Jadweli 2.0: Idadi ya Waathirika ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Mwaka 2025**

| Wilaya | Wizi wa Watoto | | Kutoa mimba | Kumpa na Kupokea ujauzito | | Usumbufu wa kingono | | Mauaji | | Uzinifu | | Jumla ya Waathirika | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'ke/Ws | W'me/Wv | W'ke/Ws | W'ke/Ws | W'me/Wv | W'ke/Ws | W'me/Wv | W'ke/Ws | W'me/Wv | W'ke/Ws | W'me/Wv | W'ke/Ws | W'me/Wv |
| Kaskazini 'A' | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 71 | 2 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 71 | 8 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 122 | 11 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 45 | 4 |
| Mjini | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 142 | 25 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 9 | 1 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 227 | 21 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 166 | 25 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 82 | 9 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 50 | 4 |
| Chake Chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 82 | 11 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 46 | 6 |
| **Jumla** | **3** | **0** | **1** | **15** | **1** | **4** | **0** | **1** | **9** | **1** | **0** | **1,104** | **126** |

**Jadweli 3.0 : Idadi ya Waathirika Wanawake na Wanaume wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, kwa Umri na Aina ya Matukio; Mwaka 2025**

| Umri | 18-24 | | 25-35 | | 36-45 | | 46-64 | | 65+ | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **W'ke** | **W'ume** | **W'ke** | **W'ume** | **W'ke** | **W'ume** | **W'ke** | **W'ume** | **W'ke** | **W'ume** | **W'ke** | **W'ume** |
| Kubaka | 36 | | 21 | | 2 | | 1 | | 0 | | 60 | |
| Kujaribu Kubaka | 2 | | 0 | | 1 | | 0 | | 0 | | 3 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 3 | | 1 | | 0 | | 0 | | 0 | | 4 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 6 | | 1 | | 0 | | 0 | | 0 | | 7 | |
| Kutorosha | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 |
| Lugha ya matusi | 9 | 0 | 9 | 1 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 20 | 2 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 24 | 0 | 11 | 0 | 10 | 2 | 4 | 0 | 1 | 0 | 50 | 2 |
| Kuingilia maharimu | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Uzinifu | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Usumbufu wa Kingono | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mauaji | 0 | 3 | 0 | 5 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 9 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 12 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 13 | 1 |
| **Jumla** | **96** | **7** | **44** | **7** | **16** | **4** | **5** | **0** | **1** | **0** | **162** | **18** |

**Jadweli 4.0: Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Muda Uliyotokea; Mwaka 2025**

| Muda Uliyotokea Matukio | 12:01 - 03:00 Asubuhi | | 03:01 - 6:00 Mchana | | 6:01 - 9:00 Jioni | | 9:01 - 12:00 Jioni | | 12:01 - 3:00 Usiku | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **W'ke/Ws** | **W'me/Wv** | **W'ke/Ws** | **W'me/Wv** | **W'ke/Ws** | **W'me/Wv** | **W'ke/Ws** | **W'me/Wv** | **W'ke/Ws** | **W'me/Wv** |
| Kubaka | 32 | | 71 | | 120 | | 160 | | 221 | |
| Kujaribu kubaka | 0 | | 2 | | 2 | | 0 | | 0 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 6 | | 7 | | 10 | | 28 | | 37 |
| Kujaribu kulawiti/Kunajisi | | 0 | | 0 | | 0 | | 1 | | 0 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 1 | | 10 | | 8 | | 12 | | 27 | |
| Kutorosha | 3 | 1 | 15 | 0 | 28 | 0 | 37 | 0 | 50 | 0 |
| Lugha ya matusi | 5 | 0 | 4 | 0 | 14 | 5 | 9 | 4 | 6 | 1 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 4 | 1 | 33 | 0 | 41 | 3 | 43 | 2 | 32 | 1 |
| Kuingilia maharimu | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Uzinifu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Usumbufu wa Kingono | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Mauaji | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 1 | 0 |
| Kutupa Watoto | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Wizi wa Watoto | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kutoa mimba | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 4 | 1 | 7 | 0 |
| **Jumla** | **46** | **9** | **137** | **7** | **219** | **19** | **269** | **38** | **345** | **40** |

**Inaendelea….Jadweli 4.0: Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Muda Uliyotokea; Mwaka 2025**

| Muda Uliyotokea Matukio | 3:01 - 06:00 Usiku | | 6:01 - 09:00 Usiku | | 09:01 - 12:00 Asubuhi | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jinsi | W'ke/Ws | W'me/Wv | W'ke/Ws | W'me/Wv | W'ke/Ws | W'me/Wv | W'ke/Ws | W'me/Wv |
| Kubaka | 46 | | 9 | | 1 | | 660 | |
| Kujaribu kubaka | 0 | | 1 | | 0 | | 5 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 7 | | 0 | | 0 | | 95 |
| Kujaribu kulawiti/Kunajisi | | 0 | | 0 | | 0 | | 1 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 9 | | 0 | | 0 | | 67 | |
| Kutorosha | 10 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 145 | 1 |
| Lugha ya matusi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 38 | 10 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 4 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 159 | 7 |
| Kuingilia maharimu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Uzinifu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Usumbufu wa Kingono | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 |
| Mauaji | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 2 | 1 | 9 |
| Kutupa Watoto | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 3 | 2 |
| Wizi wa Watoto | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 |
| Kutoa mimba | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 15 | 1 |
| **Jumla** | **71** | **7** | **13** | **4** | **4** | **2** | **1,104** | **126** |

## Zingatia Maelezo

Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Kitendochochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi auya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa , Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wangono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile nashambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hiiya mwaka 2004. Sheria hii imetungwapamoja na mambo mengine kuyafanya baadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenyeshehemu ya kumi na tatu (Section thirteen)ya sheria ya adhabu imejumuisha makosa mengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendovya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyohaviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishajiwa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wakijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadikifungo cha maisha.

**Kwa Ufafanuzi zaidi Tafadhali Wasiliana na:-**


**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**
Sanduku la Barua,2321,
Simu: +255242231869
Barua pepe: cgs@ocgs.go.tzWebsite:
http://www.ocgs.go.tz

**MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR**
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.comNukushi:
024223136
**MMP, Zanzibar.**